

**JAMHURI YA MUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA AFYA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**



**MWONGOZO WA UTOAJI HUDUMA KWA WAGONJWA WA COVID-19**

**KWENYE VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA NCHINI**

**Toleo la Kwanza Tarehe 26 Mei, 2020**

**UTANGULIZI.**

Mwenendo wa ugonjwa wa Homa kali ya Mapafu Covid 19 unaonesha kuwepo kwa wagonjwa takribani maeneo yote nchini katika viwango tofauti tofauti. Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009, inaelekeza taratibu za kudhibiti magonjwa ya kuambukiza ili kuzuia maambukizi kuongezeka. Taratibu za awali ambazo zimekuwa zikitumika tangu mwanzo wa Mlipuko wa Ugonjwa wa COVID -19 nchini zililenga kutenga wagonjwa katika maeneo maalumu ya kutolea huduma ndani (Holding facilities/rooms na nje ya Hospitali (HIDTUs). Hata hivyo kutokana na kuendelea kuwepo kwa wagonjwa wa COVID-19 mionganoni mwa wagonjwa wengine na wenyewe kuhitaji huduma zingine zikiwemo huduma za kibingwa imeonekana ni vema hospitali zote nchini zikawa na utaratibu wa kutenga wodi maalumu ndani ya hospitali zao ili kurahisisha utoaji huduma kwa wagonjwa

**Hivyo basi kila hospitali inatakiwa kutekeleza yafuatayo;**

1. Kuanzisha sehemu maalumu au wodi kwa ajili ya matibabu kwa wagonjwa wenyewe maambukizi ya Homa kali ya mapafu COVID-19.
2. Wodi za wagonjwa wa COVID-19 zinatakiwa kufuata mtiririko mzuri ili kutenganisha wagonjwa wa COVID-19 na wagonjwa wa magonjwa mengine ili kuepusha maambukizi ndani ya Hospitali.

3. Watoa huduma wapewe mafunzo ya utoaji huduma kwa wagonjwa wa COVID-19 ikiwemo IPC ili kuepusha maambukizi.
4. Kuwepo na utaratibu wa kutoa mafunzo kwa watumishi wote wa hospitali ili waweze kufanya kazi katika wodi za wagonjwa wenye maambukizi ya COVID-19.
5. Wagonjwa wenye magonjwa sugu na maambukizi ya COVID-19, wanaohitaji huduma za kibingwa, wapewe huduma hizo na wataalamu husika kwa kushirikiana na wanaotoa huduma kwa Wagonjwa wa COVID-19 (**Consultations**).
6. Pasiwepo na ubaguzi wa mgonjwa yoyote katika kupokelewa na kupewa huduma kwa sababu ni mhiswa au anajulikana kuwa na maambukuzi ya CPVID-19
7. Utoaji sampuli, ufanyywe na Wataalamu waliopo kwenye vituo vya utoaji huduma waliopewa mafunzo badala ya kusubiri timu za Mkoa na Wilaya.
8. Wagonjwa ambao ni wahisiwa wa COVID-19 waanzishiwe huduma pasipo kusubiri majibu ya vipimo vya COVID-19. Lengo ni kupunguza ucheleweshaji wa huduma kwa wagonjwa.
9. Kuwe na utaratibu maalumu waufuatiliaji wa Wagonjwa walioruhusiwa kutoka kwenye Vituo hivyo vya matibabu wakiwemo Wagonjwa wenye dalili ndogondogo (*mild cases*) na wenye magonjwa ya muda mrefu, sambamba na uwepo wa Kliniki Maalumu.
10. Taratibu za utoaji huduma kwa Wagonjwa wa COVID-19 zitafuata Miongozo iliyoaandaliwa na Wizara.
11. Taarifa za wagonjwa zitaendelea kutolewa kwa kufuata utaratibu uliopo kwa kumhusisha Mganga Mkuu wa Mkoa husika.
12. Kituo cha kutolea huduma kihakikishe kinafanya **auditing** ya kila kifo kinachotokea kinachohusiana na maambukizi ya COVID-19.
13. Endapo mhiswa (suspect) atapoteza Maisha sampuli ichukuliwe mapema iwezekanavyo, mwili uandaliwe kwa kufuata taratibu za IPC na kisha ndugu wa marehemu wakabidhiwe na kupewa maelekezo ya kuchukua tahadhari ili waendelee na taratibu za mazishi. Ndugu

wanaweza tu kusubiri majibu **kwa hiari yao** lakini pasiwepo na ulazima kutoka kwa watoa huduma.

Waganga Wakuu wa Mikoa, Wilaya, Taifa, hospitali za kanda na wafawidhi wa Hospitali zote nchini, za umma na binafsi wanaelekezwa kusimamia utekelezaji wa utaratibu huu, ambao utaendelea kutumika mpaka hapo Wizara itakapotoa maelekezo mengine.



Prof. Abel N. Makubi  
**MGANGA MKUU WA SERIKALI.**